# MAMLAKA YA ELIMU YA MAFUNZO YA UFUNDI STADI
# BARUA YA KUJIUNGA NA CHUO
# DODOMA RVTSC
# 2025

**simu**: 026 232 4154

S.L.P 2197
**Dodoma.**

**Nukushi:** 026 232 2275

dodomarvtsc@veta.go.tz

Kumb. Na. Tarehe: ………………………..

Ndugu ………………………………………………………………………………..,

**YAH: KUCHAGULIWA KUJIUNGA NA MAFUNZO YA UFUNDI STADI CHUO CHA DODOMA MWAKA- 2025**
**MAELEZO HAYA YASOMWE KWA MAKINI NA MZAZI/MLEZI WA MWANAFUNZI**

1. Unafahamishwa kwamba umechaguliwa kujiunga na chuo tajwa hapo juu katika fani ya ………………………………………………………………………………………… ngazi ya **Kwanza (**Level I**)-Kutwa/Bweni**
2. Mafunzo yatachukua muda wa miaka miwili - mitatu (2-3)
3. Chuo kitafunguliwa rasmi tarehe **13/01/2025**
4. Unatakiwa kuthibitishwa na daktari wa serikali kuwa unayo afya nzuri ya kumudu mafunzo katika fani uliyopangiwa. **Eleza ukweli kuhusu afya yako ,ili uweze kushauriwa kulingana fani uliyochaguliwa**. Ikigundulika ulidanganya utafukuzwa chuoni hata kama ulishasajiliwa. Wazazi/Walezi/Wafadhili zingatieni hili.
5. Unatakiwa kuthibitisha wewe mwenyewe na mzazi/mlezi/mdhamini wako kwamba unakubali nafasi ya mafunzo uliyopangiwa.
6. Unatakiwa kufuata sharia na taratibu zote za chuo zilizoambatanishwa kwenye barua.
7. Unatakiwa kufika chuoni na barua hii siku ya kuanza mafunzo.
8. Unatakiwa kununua vifaa vilivyoambatanishwa na barua hii kwa matumizi yako chuoni.
9. Unatakiwa kulipa kiasi cha fedha kama kilivyoambatanishwa na barua hii.
10. Hutapokelewa chuoni iwapo utafika bila kutekeleza vifungu vilivyotajwa hapo juu. Lipa mapema ili uweze kusajiliwa. **Fedha ikilipwa hairudishwi**. Kama fedha za tahadhari (Caution money) hazikutumika zitarudishwa.
11. Nafasi yako itapotea kama utashindwa kuripoti **wiki mbili** baada ya tarehe ya kufungua chuo.

______________________________

**Deodatus S. Orotha**
**MKUU WA CHUO**

**MAMLAKA YA ELIMU NA MAFUNZO YA UFUNDI STADI (VETA)**
**CHUO CHA MAFUNZO YA UFUNDI NA HUDUMA - DODOMA**

**MAELEKEZO MUHIMU.**

**1. Mahitaji muhimu kwa mafunzo ya nadharia na vitendo**

1.1 **Mashati** mawili (2) meupe (mikono mifupi) ya Tetron. Mwanafunzi aje na hayo mashati.
1.2 Suruali mbili za rangi ya bluu **(*Zitapatikana chuoni, bei yake ipo katika kiambatisho namba 3)*.**
1.3 Jozi moja ya viatu vyeusi vya ngozi, visigino vifupi vya kamba
1.4 Vifaa vya hesabu (mathematical set).
1.5 Daftari 10 kubwa (Quire 2 na kuendelea)
1.6 Kalamu za wino za kuchorea (Drawing pens) - 0.25, 0.35, 0.5, 0.7, adjustable *set square* na *Lettering Stencil* kwa (**Wanafunzi wa Uchoraji (Civil Draughting) tu**).
1.7 Karatasi nyeupe A4 (Vista Plus) au (Nopa) rimu moja kwa ajili ya mitihani.
1.8 Sweta rangi ya bluu (blue).
*1.9* Viatu vya usalama (Safety boots) – (***Zinapatikana chuoni, bei yake ipo katika kiambatisho namba 3)***
*1.10* Ovaroli/vazi rasmi la fani *(**Zinapatikana chuoni, bei yake ipo katika kiambatisho namba 3)***
1.11 T-Shirt ***(Zinapatikana chuoni, bei yake ipo katika kiambatisho namba 3)***
1.12 Kwa wanafunzi wa **Meat Processing Technology** waje na Visu viwili, apron nyeupe, Helment nyeupe na Gum boot nyeupe *(Wakachukue maelezo ya kina ya vifaa tajwa kwenye karakana ya fani ya nyama hapa chuoni).*
1.13 **Muhimu:** Wanafunzi waliochaguliwa katika fani za Food Production, House Keeping, Secretarial & Computer, Motor Vehicle Mechanics, Electrical Installation, Electronics, Civil Draughting na Road Construction & Maintenance watatakiwa kuja na nakala ya cheti cha kumaliza kidato cha nne.

**2. Ada ya mafunzo:**

2.1 Ada ya mafunzo ni Tsh **60,000 kwa wanafunzi wa kutwa** na **120,000 kwa wanafunzi wa bweni kwa mwaka. Ada ya mtihani wa taifa ni Tsh 25,000/=.** Namna ada itakavyolipwa na mahitaji mengine yanayotakiwa kwa ajili ya mafunzo yamefafanuliwa kwenye kiambatanisho namba 3 kilicho nyuma ya maelezo haya.

2.2 Ada ya chuo na ada ya mtihani ni ada mbili tofauti hivyo zitalipwa kwa control namba mbili tofauti, ada ya chuo italipwa kwa control namba inayopatikana chuoni. Ada ya mtihani italipwa ofisi za VETA kanda ya kati na control namba yake itapatikana katika ofisi hizo muhula wa pili.

2.3 Ada ya mtihani italipwa muhula wa pili wa mafunzo.

2.4 **Fedha ikishalipwa hairudishwi**. Kama fedha za tahadhari (caution money) hazikutumika zitarudishwa**.**

**3. Mahitaji ya bweni**:
Mwanafunzi wa bweni aje na mto, shuka 2 na foronya za **BLUU** kwa wavulana na shuka 2 za **PINKI** na foronya yake kwa wasichana, blanketi, chandarua, bakuli, sahani, kikombe na kijiko, pamoja na ndoo au beseni la kuogea pamoja na vifaa vya usafi binafsi.

4. **Sheria na miongozo ya chuo**
   4.1 Unatakiwa kufuata sheria na taratibu zote za chuo zilizoambatishwa kwenye barua hii kwenye kiambatisho namba 4.
   4.2 Ukichelewa kuripoti chuoni wiki mbili baada ya chuo kufunguliwa nafasi yako itafutwa na kuchukuliwa na mtu mwingine bila kukutaarifu.

5. **Mafunzo ya viwandani**

   Wanafunzi wanatakiwa kwenda kwenye mafunzo viwandani (Field/Industrial Training), kwa muda wa miezi miwili-hadi mitatu kutegemeana na fani yake. Hivyo, Mzazi atawajibika kumgharamia mwanae gharama za chakula na mahitaji mengine ili kumuwezesha kijana kupata mafunzo kwa vitendo bila usumbufu.

6. **Viambatisho:-**

   1. Muundo wa malipo mbalimbali
   2. Fomu ya uchunguzi wa afya.
   3. Fomu ya kukubali nafasi.
   4. Sheria za Chuo

7. **MENGINEYO: (Kwa hiari ya mwanachuo na mdhamini wake)**

   Pamoja na kozi ambayo umechaguliwa hapo juu, chuo kinatoa mafunzo yafuatayo baada ya saa za masomo, kwa wale wanaopenda kujiendeleza zaidi.

   - Computer Training: kujiandikisha 5,000/= Ada shilingi 235,000/= Jumla shilingi 240,000/=
   - Kozi ya udereva: kujiandikisha 5,000/=. Ada shilingi 155,000/=, kitabu 10,000/= jumla shilingi 170,000/=. **Hii ni ya muhimu sana kwa kozi za Ujenzi na matengenezo ya barabara na utengenezaji wa magari (Motor Vehicle Mechanics)**
   - Na kozi nyinginezo ambazo utazikuta chuoni.

**MAELEZO MENGINE UTAELEZWA UFIKAPO CHUONI**

Kiambatanisho (1)

## MAMLAKA YA ELIMU NA MAFUNZO YA UFUNDI STADI (VETA)

## FOMU YA KUKUBALI NAFASI YA MAFUNZO YA UFUNDI STADI

**(a) MWANACHUO**

Mimi ………………………………………………………………..………………… ninakubali nafasi ya mafunzo katika fani niliyopangiwa, pamoja na kuzingatia sheria na kanuni za chuo ambazo nimezisoma na kuzielewa vizuri.

***Sahihi: …………………………………… Tarehe: ………………………………….***

**(b) MDHAMINI/MZAZI**

Mimi ………………………………………………………… wa S. L. P ……………………………… Ninathibitisha kuwa ninamdhamini aliyetajwa hapo juu na nitamlipia gharama zote za mafunzo (ada) na michango mingine. Pamoja na nauli wakati wa kwenda Chuoni na kurudi nyumbani kwa likizo na baada ya mafunzo kama ilivyoelekezwa katika maelezo ya kujiunga na chuo wakati wote wa mafunzo.

***Tarehe: ………………………………. Sahihi: ……………………………………***

Kiambatisho (2)

# VOCATIONAL EDUCATION AND TRAINING AUTHORITY

**The Medical Officer** **Date: …../…../………..**

……………………………………………

……………………………………………

……………………………………………..

……………………………………………..

**REQUEST FOR MEDICAL EXAMINATION:**

Name of Trainee ……………………………………………………………………………………………..

Please examine the above named trainee on his/her fitness to undergo training and subsequently work as a/an ……………………………………………………………………………….

i) Eyesight …………………………………………………….

ii) Hearing …………………………………………………….

iii) Asthma …………………………………………………….

iv) Other serious diseases …………………………………………………….

v) Pregnancy test …………………………………………………….

**Medical certificate:**

I have examined the above named and consider that he/she is physically fit/unfit for training as above.

***Date: …………… Designation: ………………….. Signature & Official Stamp: ………………***

**Kiambatisho (3)**

**MAMLAKA YA ELIMU NA MAFUNZO YA UFUNDI STADI (VETA)**
**CHUO CHA MAFUNZO YA UFUNDI NA HUDUMA - DODOMA**

**MUUNDO WA MALIPO YA ADA YA MWAKA 2024/2025 KWA KILA FANI**

**Angalizo:**

Ada ya chuo na ada ya mtihani ni ada mbili tofauti hivyo zitalipwa kwa control namba mbili tofauti. Ada ya chuo italipwa kwa control namba inayopatikana chuoni na ada ya mtihani italipwa ofisi za VETA kanda ya kati na control namba yake itapatikana katika ofisi hizo.

## 1. MCHANGANUO WA ADA NA MAHITAJI MENGINE KWA WANAFUNZI WA KUTWA (DAY)

| NA | *MAHITAJI* | | FANI | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | | | FP,FO, HK, FBSS, SC | MB,CJ,PS, PPF,CD | EI, ELEC | WF,FM | MVM, RCM | MPT |
| 1 | ADA KUTWA | | 60,000 | 60,000 | 60,000 | 60,000 | 60,000 | 60,000 |
| 2 | BADGE/NEMBO | | 4,000 | 4,000 | 4,000 | 4,000 | 4,000 | 4,000 |
| 3 | MATIBABU -NHIF | | 50,400 | 50,400 | 50,400 | 50,400 | 50,400 | 50,400 |
| 4 | KITAMBULISHO | | 2,000 | 2,000 | 2,000 | 2,000 | 2,000 | 2,000 |
| 5 | MTIHANI WA TAIFA | | 25,000 | 25,000 | 25,000 | 25,000 | 25,000 | 25,000 |
| 6 | PESA YA TAHADHARI | | 10,000 | 10,000 | 10,000 | 10,000 | 10,000 | 10,000 |
| 7 | SURUALI MBILI | | 50,000 | 50,000 | 50,000 | 50,000 | 50,000 | 50,000 |
| 8 | PICHA | | 2,000 | 2,000 | 2,000 | 2,000 | 2,000 | 2,000 |
| 9 | VIATU VIGUMU | | 0 | 75000 | 75000 | 75000 | 75000 | 0 |
| 10 | OVEROLL/VAZI RASMI LA FANI | | 55,000 | 30,000 | 30,000 | 30,000 | 30,000 | 55,000 |
| 11 | T-SHIRT | | 15,000 | 15,000 | 15,000 | 15,000 | 15,000 | 15,000 |
| 12 | MICHEZO | | 10,000 | 10,000 | 10,000 | 10,000 | 10,000 | 10,000 |
| 13 | MAHAFALI | | 20,000 | 20,000 | 20,000 | 20,000 | 20,000 | 20,000 |
| | **JUMLA YA MALIPO** | | **303,400** | **353,400** | **353,400** | **353,400** | **353,400** | **303,400** |
| **Malipo Muhula wa 1** | | | **258,400** | **308,400** | **308,400** | **308,400** | **308,400** | **258,400** |
| **Malipo ya Muhula 2** | | **Ada ya chuo** | 30,000.00 | 30,000.00 | 30,000.00 | 30,000.00 | 30,000.00 | 30,000.00 |
| | | **Ada ya mtihani** | 25,000.00 | 25,000.00 | 25,000.00 | 25,000.00 | 25,000.00 | 25,000.00 |
| | | **Jumla** | **55,000.00** | **55,000.00** | **55,000.00** | **55,000.00** | **55,000.00** | **55,000.00** |

**Kirefu cha vifupisho vya fani tajwa hapo juu**

FO = Front Office
HK = House Keeping
FBSS = Food Beverage Services and Sales
FP = Food Production
MB = Masonry and Brick Laying
PS = Painting and sign writing
CJ = Carpentry and Joinery
EI = Electrical Installation
ELEC = Electronics
SC = Secretarial & Computer
PS = Painting & Sign writing
WF = Welding & Fabrication
FM = Fitter Mechanics
MVM = Motor Vehicle Mechanics
MPT = Meat Processing Techn
PPF = Plumbing & Pipe Fitting
CD = Civil Draughting
RCM = Road Construction & Maintenance

## MCHANGANUO WA ADA NA MAHITAJI MENGINE KWA WANAFUNZI WA BWENI

<table>
<tr><th rowspan="2">NA</th><th rowspan="2">MAHITAJI</th><th colspan="6">FANI</th></tr>
<tr><th>FP,FO,<br>HK,<br>FBS, SC</th><th>MB,CJ,PS,<br>PPF,CD</th><th>EI, ELEC</th><th>WF,FM</th><th>MVM, RCM</th><th>MPT</th></tr>
<tr><td>1</td><td>ADA.</td><td>120,000</td><td>120,000</td><td>120,000</td><td>120,000</td><td>120,000</td><td>120,000</td></tr>
<tr><td>2</td><td>GODORO</td><td>10,000</td><td>10,000</td><td>10,000</td><td>10,000</td><td>10,000</td><td>10,000</td></tr>
<tr><td>3</td><td>MATIBABU-NHIF</td><td>50,400</td><td>50,400</td><td>50,400</td><td>50,400</td><td>50,400</td><td>50,400</td></tr>
<tr><td>4</td><td>SURUALI MBILI</td><td>50,000</td><td>50,000</td><td>50,000</td><td>50,000</td><td>50,000</td><td>50,000</td></tr>
<tr><td>5</td><td>VIATU VIGUMU</td><td>0</td><td>75000</td><td>75000</td><td>75000</td><td>75000</td><td>0</td></tr>
<tr><td>6</td><td>OVEROLL/VAZI RASMI</td><td>55,000</td><td>30,000</td><td>30,000</td><td>30,000</td><td>30,000</td><td>55,000</td></tr>
<tr><td>7</td><td>T-SHIRT</td><td>15,000</td><td>15,000</td><td>15,000</td><td>15,000</td><td>15,000</td><td>15,000</td></tr>
<tr><td>8</td><td>BADGE/NEMBO</td><td>4,000</td><td>4,000</td><td>4,000</td><td>4,000</td><td>4,000</td><td>4,000</td></tr>
<tr><td>9</td><td>KITAMBULISHO</td><td>2,000</td><td>2,000</td><td>2,000</td><td>2,000</td><td>2,000</td><td>2,000</td></tr>
<tr><td>10</td><td>PICHA</td><td>2,000</td><td>2,000</td><td>2,000</td><td>2,000</td><td>2,000</td><td>2,000</td></tr>
<tr><td>11</td><td>MTIHANI WA TAIFA</td><td>25,000</td><td>25,000</td><td>25,000</td><td>25,000</td><td>25,000</td><td>25,000</td></tr>
<tr><td>12</td><td>PESA YA TAHADHARI</td><td>10,000</td><td>10,000</td><td>10,000</td><td>10,000</td><td>10,000</td><td>10,000</td></tr>
<tr><td>13</td><td>MICHEZO</td><td>10,000</td><td>10,000</td><td>10,000</td><td>10,000</td><td>10,000</td><td>10,000</td></tr>
<tr><td>14</td><td>MAHAFALI</td><td>20000</td><td>20000</td><td>20000</td><td>20000</td><td>20000</td><td>20000</td></tr>
<tr><td colspan="2">JUMLA</td><td>373,400</td><td>423,400</td><td>423,400</td><td>423,400</td><td>423,400</td><td>373,400</td></tr>
<tr><td colspan="2">Malipo ya Muhula wa 1</td><td>288,400</td><td>338,400</td><td>338,400</td><td>338,400</td><td>338,400</td><td>288,400</td></tr>
<tr><td rowspan="3">Malipo ya Muhula wa 2</td><td>Ada ya chuo</td><td>60,000</td><td>60,000</td><td>60,000</td><td>60,000</td><td>60,000</td><td>60,000</td></tr>
<tr><td>Ada ya mtihani</td><td>25,000.00</td><td>25,000.00</td><td>25,000.00</td><td>25,000.00</td><td>25,000.00</td><td>25,000.00</td></tr>
<tr><td>Jumla</td><td>85,000</td><td>85,000</td><td>85,000</td><td>85,000</td><td>85,000</td><td>85,000</td></tr>
</table>

- Malipo ya ada, Godoro, nembo, pesa ya tahadhari, michezo, ada ya udereva na kitambulisho yalipwe kwenye akaunti ya serikali kwa control namba ambayo utapewa na mhasibu wa chuo ukifika chuoni.

- **Suruali, T-shirts, Overoll/Vazi rasmi la fani, viatu vigumu na picha vitapatikana chuoni kwa bei zilizooneshwa kwenye jedwali hapo juu. Utaelekezwa namna ya kulipa malipo haya wakati wa usajiIi.**

- Kila mwanafunzi atalipa malipo ya BIMA ya afya ya NHIF. Chuo kitaanda utaratibu kwa wanafunzi kupata control namba ili wanafunzi wenyewe waweze kuzitumia kulipia huduma hii muhimu, hivyo kila mwanafunzi aje na pesa kwa lengo hilo. Wanafunzi wote kwa pamoja na mapema kabisa watawezeshwa kulipia haraka huduma hii muhimu.

- **Kila mwanafunzi anatakiwa kuwa na kitambulsho cha Taifa**. Kitambulisho hiki kitamsaidia mwanafunzi kupata huduma nyingi zinazohitaji kitambulisho, moja ya kusudio kubwa la kuwataka wanafunzi kuwa na kitambulisho hiki ni ili waweze kupata BIMA ya afya. **Bila kitambulisho cha Taifa mwanafunzi hawezi kupata BIMA ya afya.**

- Malipo ya pesa ya mtihani wa taifa yatalipwa kwa control number inayotolewa katika ofisi za VETA kanda ya kati na malipo haya yatalipwa muhula wa pili wa mafunzo.

Mwanafunzi asisite kuuliza swali lolote endapo atapata ugumu wa kushughulikia suala la ulipaji wa ada na mahitaji mengine awapo chuoni na asifanye kitu ambacho hajakielewa
Kiambatanisho (4)

## MAMLAKA YA ELIMU NA MAFUNZO YA UFUNDI STADI (VETA)
### CHUO CHA MAFUNZO YA UFUNDI NA HUDUMA - DODOMA

## SHERIA ZA CHUO KWA WANAFUNZI WA KUTWA NA BWENI

**ILI KUFANIKISHA MAFUNZO YA AWALI YA UFUNDI KILA MWANAFUNZI ANATAKIWA KUFUATA SHERIA ZIFUATAZO:-**

### 1. MAHUDHURIO

(a) Kila mwanafunzi anatakiwa kufika chuoni kabla ya saa 1.20 asubuhi. Hii ina maana ifikapo saa 1.20 wanafunzi wote wawe wameshafika chuoni. **Atakaye chelewa hataruhusiwa kuingia chuoni.**

(b) Mwanafunzi hatakiwi kutoka nje ya chuo kwenda nyumbani, hospitali au sehemu nyingine yoyote ile bila ya kuruhusiwa na mwalimu (Mkuu wa fani)

(c) Mwanafunzi apatapo matatizo ya msiba, kuuguliwa au kuugua mwenyewe ni lazima habari/taarifa zifike chuoni, **bila ya kufanya hivyo ni kosa**.

(d) Mahudhurio chini ya 85% mwanafunzi hataruhusiwa kufanya mitihani.

(e) Vyumba/madarasa na vifaa vitumiwe kufuatana na shughuli zake. Hairuhusiwi kuchora au kuandika kwenye kuta za majengo ya Chuo.

### 2. MAVAZI

(a) Sare ya chuo ni suruali ya Bluu na shati Jeupe mikono mifupi. Sare hiyo ivaliwe wakati wote mwanafunzi awapo chuoni na wakati wa safari ya kuja chuoni na kurudi nyumbani. **Wakati wote shati liwe limechomekewa.** Ni marufuku kuvaa nguo za kubana. **Ni marufuku kupunguza vipimo vya suruali. Ukipunguza vipimo vya suruali utashona nyingine.** Siku za **Jumatano** na **Ijumaa** sare ni T-SHIRT na suruali ya chuo.

(b) Ovaroli livaliwe wakati wa vipindi vya kazi za mikono tu.

(c) Viatu vyenye visigino virefu na kandambili au sandosi (sandals) haviruhusiwi kuvaliwa chuoni wakati wa masomo.

(d) Mkanda wa suruali uwe MWEUSI wa ngozi na usiwe na urembo

### 3. USAFI WA MWILI

(a) Hairuhusiwi kuvaa hereni, pete, bangili, mkufu na mapambo ya aina yoyote ile kwa kipindi chote cha mafunzo.

(b) Hairuhusiwi kutumia vipodozi au manukato yanayotoa harufu kali.

(c) **Nywele kwa wavulana**

- (i) Zikatwe ziwe fupi sana, KIPARA, KIDUKU, PANKI hairuhusiwi kabisa.
- (ii) Ndevu, na Mustachi haviruhusiwi

(d) **Nywele kwa wasichana**

- (i) Zikatwe ziwe fupi au zisukwe kwa mistari mitano au sita ya kurudi nyuma.

(e) **Kucha zisifugwe kabisa wala kupaka rangi.**

**4. WIZI WA MALI ZA CHUO AU MALI YA MTU YEYOTE YULE:**

(a) Vitendo vyovyote vya wizi haviruhusiwi. Pindi ikibainika mwanafunzi ameiba mali ya chuo au ya mwanafunzi mwenzake, hatua za kisheria zitachukuliwa mara moja.

(b) Ukipoteza vifaa vya chuo utatakiwa kulipa gharama kamili ya vifaa ama ukakinunue kifaa chenyewe kilicho potea.

(c) Hairuhusiwi mwanafunzi kuingia na kifaa chochote kile kinachofanana na vile vilivyoko ndani ya chuo.

(d) Mwanafunzi atapekuliwa wakati wa kutoka karakana na getini.

**5. UGOMVI:**

Ugomvi, kupigana na kushambuliana ni makosa ya jinai. Atakayepatikana akijihusisha na matendo ya namna hiyo hatua za kisheria zitachukuliwa mara moja.

**6. ULEVI:**

Iwapo itabainika mwanafunzi analewa, au kuonekana katika sehemu za kileo, anavuta bangi au madawa ya kulevya hatua za kisheria zitachukuliwa mara moja.

**7. MAPENZI:**

(a) Uhusiano wa kimapenzi chuoni kati ya mwanafunzi na mwanafunzi au kati ya mfanyakazi na mwanafunzi hairuhusiwi kabisa.

(b) Mwanafunzi wa kiume au wa kike haruhusiwi kuingia maeneo wanayoishi wafanyakazi wa chuo bila kibali au ruhusa.

**8. MIGOMO:**

Migomo ni marufuku, na kuchochea migomo ni kosa lisilostahimilika. Atakayeshawishi au kusababisha migomo hatua za kisheria zitachukuliwa mara moja.

**9. LUGHA:**

Lugha inayotumika kuendeshea masomo ni **kiingereza** hivyo ni wajibu wa kila mwanafunzi kujifunza kiingereza.

**10.** Jina lisibadilishwe mpaka ziwepo sababu na hati maalum kwa uthibitisho na ajulishwe Mkuu wa Chuo mara moja.

**11.** Ni **MARUFUKU** kwa mwanachuo kuja na **simu za mkononi**. Ikigundulika una simu au simu ikiita wakati wa vipindi utanyang'anywa na itaifadhiwa mpaka utakapomaliza chuo.

## ONGEZEKO LA SHERIA KWA MWANACHUO WA BWENI

12. Mwanachuo ataruhusiwa kutoka nje ya Chuo siku zifuatazo tu:-

(i) Jumapili tangu saa 12.00 asubuhi hadi saa 12.00 jioni

(ii) Jumamosi tangu saa 7.30 mchana hadi saa 12.00 jioni

Hairuhusiwi kutoka nje ya chuo wakati wowote bila sare na kibali maalum.

13. Mwanachuo yeyote anayeruhusiwa kutoka nje ya eneo la Chuo anapaswa kuwa na kitambulisho cha Chuo, sare ya Chuo na atajiandikisha lango kuu. Mwanafunzi

atakayeonekana nje ya maeneo ya Chuo bila kuwa na sare atachukuliwa hatua kali za kinidhamu ikiwa ni pamoja na kunyang'anywa nafasi ya kulala bwenini au kufukuzwa chuoni.

14. Mwanafunzi atakayepatikana na kosa la kulala au kuwa nje ya chuo bila kibali atasimamishwa masomo na kufukuzwa bwenini.

15. Haitaruhusiwa kupikia chakula bwenini, na atakayekiuka sheria hii atachukuliwa hatua kali.

16. (a) Ni marufuku wanachuo wa kiume na wakike kutembeleana mabwenini.

    (b) Hairuhusiwi **KABISA** kwa mwanachuo kuingia katika eneo wanamoishi wafanyakazi wa chuo bila ruhusa au kibali.

17. **Hairuhusiwi kupeleka chakula bwenini**. Endapo kuna mgonjwa, ruhusa maalum kutoka kwa mwalimu wa zamu/warden itatolewa.

18. Taa za madarasani na mabwenini zizimwe saa 4:00 za usiku.

19. Hakuna ruhusa kumkaribisha au kumlaza mgeni, ikiwa mwanachuo atatembelewa na mgeni au ndugu siku ya masomo ni lazima kumjulisha mwalimu wa zamu kabla ya kumkaribisha katika sehemu ya mazungumzo.

    ⇨ Wageni wanaruhusiwa kuwatembelea ndugu zao kila Jumamosi kuanzia saa 7:00 mchana hadi saa 12:00 jioni.

    ⇨ Kila Jumapili na siku za sikukuu kuanzia saa 12:00 asubuhi mpaka 12:00 jioni.

20. Vyumba/Madarasa na vifaa vitumiwe kufuatana na shughuli zake. Hairuhusiwi kuchora au kuandika kwenye kuta za majengo ya chuo.

21. Mwanafunzi wa bweni haruhusiwi kulala nje ya Chuo. Iwapo ikitokea dharura ya kulala nje ya chuo, ruhusa itatolewa na ofisi ya Mkuu wa Chuo.

22. Ruhusa ya kutoka Chuoni; Jumamosi saa 7:30mchana hadi saa 12:00 jioni. Jumapili na siku za sikukuu saa 12 asubuhi hadi saa 12:15 jioni; majina yaandikwe kwenye kitabu cha kutoka na kuingia. Mhusika aweke muda wa kutoka na kusaini arudipo.

23. Mwanafunzi atakayegundulika kuwa **hajui** kusoma, kuandika na kuhesabu atashauriwa kujiunga na kozi fupi badala ya kozi ndefu. Hivyo mzazi/mlezi/mfadhili atalazimika kulipa upya gharama za kozi fupi.

# Karibu sana VETA Dodoma

**MKUU WA CHUO**